AOC-495 Doc. Code: GPF
Toleo 7-26
Ukurasa wa 1 kati ya 2

Jimbo la Kentucky
Mahakama ya Haki *www.kycourts.gov*
RCr 8.08, 8.10
KRS 189A.010; 189A.070; 189A.085

**DUI (Guilty Plea)**

**Kuendesha ukiwa umetumia kilevya (Kukubali Hatia)**

Namba ya Kesi ________________
Mahakama ya ________________
Wilaya ________________
Mashtaka Namba: ________________
Tarehe ya tukio ________________

JIMBO LA KENTUCKY — MDAI
DHIDI YA

________________________________________ — MDAIWA

ANUANI: ________________________________________

________________________________________

Mdaiwa akiwepo pamoja na ❑ wakili wake AU ❑ bila wakili, na akiiomba mahakama hii kumruhusu kutoa ombi la **KUKUBALI HATIA** yake kama inavyoonyeshwa hapa chini. Katika kukubaliana na hoja hiyo, Mdaiwa anasema ya kwamba:

1. Mimi ndiye niliyetajwa hapo juu kwenye mashtaka/hati **inayonishtaki** kwa kosa la **kuendesha chombo wakati umetumia kilevya, ❑ ikiwa ni kosa la kwanza ❑ la pili ❑ la tatu ❑ la nne au kosa la zaidi ya hapo.** Ninakubali hatia ya _____________.
2. Maamuzi yangu hayajadhurika kwa matumizi ya madawa ya kulevya, pombe, au dawa zozote.
3. Nimepitia nakala ya mashataka yangu.
4. ❑ **Nimemueleza wakili wangu ukweli wote unaohusiana na mashtaka yangu**. Ninaamini ana taarifa kamili kuhusiana na kesi yangu. Tumejadiliana kikamilifu na ninaelewa mashataka dhidi yangu na utetezi unaowezekana juu yake. Nimeridhika na ushauri niliopewa na wakili wangu.
5. **Naelewa kuwa naweza "KUKUBALI HATIA" au "KUKATAA HATIA" kwenye makosa yoyote dhidi yangu. Ninaielewa** kuwa Katiba **inanihakikishia haki zifuatazo:** (a) haki ya kutokotoa **ushahidi dhidi yangu;** (b) haki ya kesi ya **haraka na ya wazi kwa kutumia baraza la mahakama, na uwakilishi wa kisheria,** ambapo serikali ya **jimbo itatakiwa kuthibitisha hatia yangu bila ya mashaka yoyote** (c) haki ya **kuteuliwa mwanasheria wa kunitete iwapo siwezi kugharamia malipo ya wakili;** (d) haki ya **kuwakabili na kuwauliza maswali mashadidi wote watakaotoa ushahidi dhidi yangu;** (e) haki ya kutoa **ushahidi wowote, ikiwa ni pamoja na kuleta mashahidi watakaotoa ushahidi wa kunitetea;** (f) haki ya kukata **rufani ili kesi yangu isikilizwe na mahakama ya juu;** na (g) haki ya kuwa na dhamana **inayokubalika.** Naelewa **kama "NIKIKUBALI HATIA," naachana na haki zote hizi na ninapoteza haki ya kuendesha chombo cha moto kwenye jimbo la Kentucky.** - Ninaelewa kwamba **kama nitapatikana na hatia ya makosa mengine ya kuendesha chombo wakati nimetumia kilevya au kwa kuendesha wakati nina makosa yanayohusiana na kusimamishwa kwa leseni, adhabu zitaongezeka kwa kila kosa nitakalotiwa hatiani.**
6. Ninaelewa kama **"NITAKUBALI HATIA",** mahakama inaweza kulazimika kunipa adhabu yoyote iliyomo ndani ya sheria na pamoja na kwamba inaweza kufikiria mapendekezo ya serikali ya jimbo, inaweza kuyakataa. Adhabu za kisheria kwa kukosa la kuendesha ukiwa umetumia kilevya ni:

   (a) **Kosa la Kwanza ndani ya miaka 10:**

   (1) **Adhabu** ni fani kati ya $200 mpaka $500 na/au kifungo cha kati ya masaa 48 na siku 30 jela. Masaa 48 mpaka siku 30 za kazi ya kwenye jamii yanaweza kubadilishwa kuwa faini au kifungo cha jela. Kama kulikuwa na mazingira ya uchochezi wakati wa tukio, kutakuwa na adhabu ya lazima ya siku zisizopungua nne (4) za kifungo.

   (2) **Gharama na Ada** - Gharama za mahakama, ada za huduma za kosa la kuendesha ukiwa umetumia kilevya, gharama za mpango wa matibabu, ada za wilaya husika, ada za jimbo.

   (3) **Mpango wa matibabu ya matatizo ya pombe au madawa ya kulevya** - Siku 90

   (4) **Leseni Imesimamishwa** - Kwa kipindi kisichozidi miezi 6 (au kama Mshitakiwa yupo chini ya miaka 18, mpaka pale Mshitakiwa atakapotimiza miaka 18, chochote kati ya hivi kitakachokuwa muda mrefu zaidi.) Atastahiki kuomba leseni ya chombo cha kuwasha gari na anaweza kustahiki kuomba leseni kwa ajili ya kukabiliana na ugumu wa maisha endapo kama uvunjaji wa sheria ulitokea chini ya KRS 189.010(1)(c) au (d). Kibati cha leseni kinaweza kuzuiliwa kama leseni ya chombo cha kuwasha gari au leseni kwa ajili ya kukabiliana na ugumu wa maisha hazitatolewa.

   (b) **Kosa la pili ndani ya miaka 10:**

   (1) **Adhabu ya faini kati ya** $350 mpaka $500 na siku 7 mpaka miezi 6 jela. Mahamaka inaweza kutoa amri ya siku 10 hadi miezi 6 ya kazi kwenye jamii. - Lazima kutumikia angalau kifungo cha jela na/au kazi kwenye jamii. Kama mazingira ya uchochezi yalikuwepo, kifungo cha lazima kitakuwa ni angalau siku 14.

   (2) **Gharama na Ada** - Gharama za mahakama, ada za huduma za kosa la kuendesha ukiwa umetumia kilevya, gharama za mpango wa matibabu, ada za wilaya husika, ada za jimbo.

   (3) **Mpango wa matibabu ya ulevi au matumizi yasiyofaa ya madawa ya kulevya** - Mwaka 1

   (4) **Leseni Imesimamishwa** - Kwa kipindi kisichozidi miezi 18 (au kama Mshitakiwa yupo chini ya miaka 18, mpaka pale atakapotimiza miaka 18, chochote kati ya hivi kitakachochukua muda mrefu zaidi.) Atastahiki kuomba leseni ya chombo cha kuwasha gari na anaweza kustahiki kuomba leseni kwa ajili ya kukabiliana na ugumu wa maisha endapo kama uvunjaji wa sheria ulitokea chini ya KRS 189.010(1)(c) au (d). Kibati cha leseni kinaweza kuzuiliwa kama leseni ya chombo cha kuwasha gari au leseni kwa ajili ya kukabiliana na ugumu wa maisha hazitatolewa.

FOR INFORMATIONAL PURPOSES ONLY. NOT AN OFFICIAL COURT DOCUMENT.
KWA AJILI YA TAARIFA TU. SIO HATI RASMI YA MAHAKAMANI.

(c) **Kosa la Tatu ndani ya Miaka10:**

(1) **Adhabu ya faini kati ya** $500 mpaka $1000 na siku 30 mpaka miezi 12 jela, na mahakama inaweza kutoa amri ya siku 10 mpaka miezi 12 ya kazi kwenye jamii. Lazima kutumikia angalau kifungo cha jela na/au kazi kwenye jamii. Kama mazingira ya uchochezi yalikuwepo, kifungo cha lazima kitakuwa ni angalau siku 60.

(2) **Gharama na Ada** - Gharama za mahakama, ada za huduma za kosa la kuendesha ukiwa umetumia kilevya, gharama za mpango wa matibabu, ada za wilaya husika, ada za jimbo.

(3) **Mpango wa matibabu ya ulevi au matumizi yasiyofaa ya madawa ya kulevya** - Mwaka 1

(4) **Leseni Imesimamishwa** - Kwa kipindi kisichozidi miezi 36 (au kama Mshitakiwa yupo chini ya miaka 18, mpaka pale atakapotimiza miaka 18, chochote kati ya hivi kitakachochukua muda mrefu zaidi.) Atastahiki kuomba leseni ya chombo cha kuwasha gari na anaweza kustahiki kuomba leseni kwa ajili ya kukabiliana na ugumu wa maisha endapo kama uvunjaji wa sheria ulitokea chini ya KRS 189.010(1)(c) au (d). Kibati cha leseni kinaweza kuzuiliwa kama leseni ya chombo cha kuwasha gari au leseni kwa ajili ya kukabiliana na ugumu wa maisha hazitatolewa.

(d) **Kosa la Nne au zaidi ndani ya Miaka 10:**

(1) **Adhabu** - Miaka 1 mpaka 5 ya kufungwa (Kosa kubwa la uhalifu Daraja la D). Lazima kutumikia kifungo kwa siku 120. Kama mazingira ya uchochezi yalikuwepo, kifungo cha lazima kitakuwa ni angalau siku 240.

(2) **Gharama na Ada** - Gharama za mahakama, ada za huduma za kosa la kuendesha ukiwa umetumia kilevya, gharama za mpango wa matibabu, ada za wilaya husika, ada za jimbo.

(3) **Mpango wa matibabu ya ulevi au matumizi yasiyofaa ya madawa ya kulevya** - Mwaka 1

(4) **Leseni Imesimamishwa** - Kwa kipindi kisichozidi miezi 60 (au kama Mshitakiwa yupo chini ya miaka 18, mpaka pale atakapotimiza miaka 18, chochote kati ya hivi kitakachochukua muda mrefu zaidi.) Atastahiki kuomba leseni ya chombo cha kuwasha gari na anaweza kustahiki kuomba leseni kwa ajili ya kukabiliana na ugumu wa maisha endapo kama uvunjaji wa sheria ulitokea chini ya KRS 189.010(1)(c) au (d). Kibati cha leseni kinaweza kuzuiliwa kama leseni ya chombo cha kuwasha gari au leseni kwa ajili ya kukabiliana na ugumu wa maisha hazitatolewa.

(e) **Mazingira ya uchochezi yanayorejewa hapo juu ni:** (1) Kuendesha gari kwa zaidi ya maili 30 kwa saa juu ya kiwango cha kasi ya mwendo kilichowekwa (2) Kuendesha gari kuelekea kinyume na mwelekeo wa barabara kuu; (3) Kuendesha gari ambalo limesababisha ajali iliyopelekea kifo au majeraha makubwa; (4) Kuendesha gari wakati kiwango cha pombe kwenye damu au pumzi ya dereva ni 0.15 au zaidi kama itakavyoonekana kwenye vipimo vya sampuli ya damu au pumzi ya dereva ndani ya masaa 2 tangu kuacha kuendesha gari; (5) Kukataa kufanyiwa vipimo vyovyote pumzi ambavyo vimeombwa na afisa ambaye ana sababu za kuridhisha kuamini kuwa dereva alikuwa anaendesha au anamiliki gari kinyume na KRS 189A.010(1), labda tu kama ni kwa kosa la kwanza chini ya KRS 189A.010(5)(a); na (6) Kuendesha gari ambamo kuna abiria chini ya miaka 12.

7. Naelewa kwamba kama **Mahakama itakataa ombi langu**, italazimika kunitaarifu na kuniruhusu ama niendelee na ombi langu la kukubali hatia, ambapo ninaweza kupata matokeo ambayo si ya kuridhisha katika kesi yangu kulinganisha na nilivyofikiria kwenye kwenye makubaliano ya ombi langu, au kuondoa ombi langu la kukubali hatia na kuendelea na kesi.

8. Kutokana na kukubali hatia, **Jimbo limekubali kupendekeza kwa** Mahakama mashtaka na hukumu za mwanzo/yaliyorekebishwa kama ifuatavyo mashata na hukumu: ______________________________
______________________________.

Zaidi ya mapendekezo haya, hakuna yeyote, ikiwa ni pamoja na mwanasheria wangu, aliyeniahidi kuwa na faida yoyote ingine kutokana na kukubali hatia, pia hakuna yeyote aliyenilazimisha kutoa ombi la **"KUKUBALI HATIA"**

9. ❑ Kwa sababu nina hatia na sijadai **kuwa sina makosa**, ningependa **"KUKUBALI HATIA"** kutegemeana na mapendekezo yaliyotolewa hapo juu. Ukweli unathibitisha hatia yangu: Kwenye tarehe ______________________________,
______________________________
______________________________

**AU**

❑ Kufuatana na Kesi ya <u>North Carolina dhidi ya Alford,</u> **400 U.S. 25 (1970)**, ningependa **"KUKUBALI HATIA"** kutegemeana na mapendekezo yaliyotolewa hapo juu. Kwa kukubali hivyo, sikubali hatia ila naamini ushahidi dhidi yangu unaonyesha hatia kwa kiasi kikubwa na maslahi yangu yatatimia kwa kukubali hatia.

10. Naelewa kuwa kutokana na kutiwa hatiani leo hii, **ninaweza kukabiliwa na adhabu kubwa/iliyoongezwa iwapo nitakuwa na hatia/au kupatikana na hatia katika matukio ya uhalifu katika siku zijazo.** Ninaelewa kuwa kama mimi siyo raia wa Marekani,ninaweza kukabiliwa na kufukuzwa kutoka nchini kutokana na sheria na kanuni zinazotawala Uhamiaji na Utekelezaji wa Forodha wa Marekani.

11. Natangaza kuwa maombi yangu ya **"KUKUBALI HATIA"** yamefanywa nikiwa huru, kwa akili yangu na kwa hiari yangu. Naelewa kwa asili ya taratibu hizi, masharti kamili ya ombi hili, na wajibu wote uliowekwa juu yangu kwa kanuni zake.

Imesainiwa kwenye mahakama ya wazi tarehe ________ mwezi wa ______________________________.

| | | |
|---|---|---|
| ______________________ | ______________________ | ______________________ |
| **Sahihi ya Mdaiwa** | **Sahihi ya Wakili wa Utetezi (kama yupo)** | **Andika Jina la Wakili** |

FOR INFORMATIONAL PURPOSES ONLY. NOT AN OFFICIAL COURT DOCUMENT.
KWA AJILI YA TAARIFA TU. SIO HATI RASMI YA MAHAKAMANI.